

## Mapendekezo

Ili kutatua kero na maswala haya ya kimsingi tunapendekeza:

1. Mipango ya uhamasishaji juu ya sheria na usimamizi wa mikoko kwa jamii izidishwe na kutiliwa mkazo.
2. Kukataza na kupunguza matumizi ya tanuru za kienyeji za chokaa kwa kuanzisha na kuzidisha matumizi ya tanuru za kisasa zinazotumia teknolojia mbadala za kuhifadhi kawi.
3. Kuzidisha uwezo na ustadi wa kusimamia maliasili kupitia mifumo ya kitaalimu.
4. Rudufu na kuongeza upanzi wa mikoko na kuboresha maeneo yaliyoharibika kupitia mipango mahususi ya serikali.
5. Serikali kuajibika na kudhibiti sera kuhusu ukataji wa mikoko.



Ofisi ya IUCN (muungano wa uhifadhi duniani) ya afrika mashariki na kusini, pamoja na CORDIO (shirika la utafiti na maendeleo ya pwani na bahari ya hindi) na EAWLS (shirika la afrika mashariki la viumbe hai porini) ziliandaa warsha mbili za jamii mwaka 2007/2008 nchini Kenya na Tanzania. Wakilishi wa jamii waliakisi na kuelezea hadhi ya mazingira ya bahari na kutoa mapendekezo thabiti ya kufanikisha rasilimali za bahari na uendeleu wa chuma riziki. Uchapishaji wa brosha hizi ni matokeo ya kazi hiyo.

Warsha za jamii ni sehemu mojawapo ya mradi mkubwa "uhifadhi kiini cha mali kwa chuma riziki katika afrika mashariki" unaofadhiliwa na IDRC (kituo cha kimataifa cha utafiti na maendeleo) na Ford Foundation. Pia mradi wa kujenga uwezo na kuimarisha sera za kuwaezesha jamii ya pwani kusimamia rasilimali zao za bahari katika afrika mashariki unaofadhiliwa na KNCF (mfuko wa fedha wa Kiedanren wa kuhifadhi viumbe). Madhumuni ya miradi hii ni kuongeza maarifa na ufahamu juu ya uhifadhi wa bioanuai unavyochangia chuma riziki na kuwasaidia jamii kudhihirisha umuhimu huu kwa wanasiasa na waundaji sera.

Maoni yaliyotolewa kwa chapisho hili si lazima kuwa mawazo ya mitizamo ya IUCN, IDRC, The Ford Foundation, KNCF, CORDIO au EAWLS.

Sifa kwa picha: M. Samoilys/CORDIO  
TCZCDP

## Kujenga Uwezo wa Jamii Kusimamia Rasilimali ya Baharini Tanzania



## Kikundi cha Kuboresha Mikoko



Na:  
Aziz A Mgeni  
Esha A Sadala  
Omari Kombo  
Wajihi Haji

## Utangulizi

Mikoko hupatikana katika sehemu nyingi kwenye ukanda wa pwani ya Tanzania

Warsha ya kitaifa ya jamii ya pwani ilifanyika Tanga kuanzia tarehe 28 hadi 31 Januari 2008. Lengo la warsha ilikuwa kuzipa

jamii za pwani fursa ya kutangamana na kubadilishana uzoefu wa usimamizi na utendaji kwenye rasilimali za baharini pamoja na kuelezea kwa ufasaha mahitaji yao. Kama wakilishi wa vikundi vya kuboresha misitu ya mikoko, tulitoa maoni yetu, malengo, shughuli masuala nyeti na mapendekezo katika mkutano huo.

## Vikundi vya kuboresha misitu na upanzi mikoko, malengo na azma yao

JINA LA KIKUNDI	SHABAHA
CHIBANDULA (Kijiji cha Msimbati, Mtwara)	<ul style="list-style-type: none"><li>Kuhakikisha wavuvi wanapata vifaa bora vya uvuvi na kuwawezesha kuvua kwenye maji ya kina kirefu badala ya uvuvi wa bahari ya kina kifupi.</li><li>Kuwaauni wanachama kupata mikopo midogo midogo pamoja na ustadi wa uvuvi endelevu, usimamizi bora wa mikoko na uhifadhi kutoka kwa mamlaka ya bahari</li></ul>
PAPA Kijiji cha Kwale, wilaya ya Mkinga (Tanga)	<ul style="list-style-type: none"><li>Kuongeza viwango vya mapato miongoni mwa jamii za pwani kupitia usimamizi endelevu wa mali asili</li><li>Tekeleza shughuli mbalimbali za uhifadhi wa mazingira; kudhibiti na kushika doria, kuboresha mikoko; uhamasishaji na kuarifu kupitia mabroscha</li></ul>
"DEEP SEA" BOMA Kamati ya usimamizi, Tanga (Samaki, mikoko na maliasili nyingine)	<ul style="list-style-type: none"><li>Uhifadhi na mazingira k.m. upanzi wa mikoko</li><li>Utalii unaohusiana na ekolojia na jamii</li><li>Kushika doria na kutathmini rasilimali</li><li>Kuchunguza na kutathmini zao la samaki, vifaa vya uvuvi na leseni.</li></ul>
CHONGOLEANI (Kikundi cha Uhifadhi Mikoko, Tanga)	<ul style="list-style-type: none"><li>Kulinda na kuhifadhi mikoko na maeneo ya mazalio ya samaki kupitia upanzi wa mikoko, na kushika doria</li><li>Kupunguza umaskini na kuongeza mapato ya fedha kupitia shughuli mbadala za kukimu maisha k.v. ufugaji wa nyuki na uzalishaji wa asali</li></ul>

## Mwelekeo wa kisasa na matumizi ya Rasilimali

- Uvunaji haramu wa mikoko, uharibifu wa maeneo ya mazalio, ongezeko la mmomonyoko wa fuo na mwambao unaosababisha maanguko ya mara kwa mara ya yaliyo karibu na ufuoni.
- Tunaona ongezeko la mahitaji ya mashua, mbao za ujenzi na kuni.
- Tunaona ongezeko la idadi ya tanuru za chokaa.
- Kuna ukosefu wa teknolojia ya kuhifadhi fueli na ukosefu wa mbao mbadala.
- Tumeona upungufu wa aina ya mikoko hususan ya ujenzi wa mashua na nyumba.

## Utendaji wa jamii juu ya matumizi endelevu ya rasilimali ya bahari

Kuna mifano mingi ya usimamizi wa rasilimali ya bahari na pwani inayoendeshwa na jamii kwa mfano, 'Tanga Coastal Zone Conservation and Development Programme (TCZCDP)' na mradi wa 'Rufiji, Mafia and Kilwa Seascape (RUMAKI)' ambayo imechangia vyema usimamizi wa kuboresha mikoko.

## Maswala kipaumbele

Ingawa kumekuwa na matukio dhahiri yaliyochangia kuleta mafanikio kwa sekta ya mikoko, mambo yanayofuata bado yanatukera.

- Ukataji kiholela wa mikoko kutokana na ongezeko la mahitaji ya kuni za tanuru za chokaa zinazomilikiwa na jamii nyingi.
- Uvunaji haramu wa rasilimali.
- Doria na tathmini pungufu pamoja na miundo hafifu wa msingi ya usimamizi wa kijamii
- Ukusanyaji wa vyambo vya samaki
- Mabadiliko ya hali ya anga, mafuriko na mashapo wakati wa El nino
- Upungufu wa uhamasishaji wa jamii juu ya sheria na sera za misitu pamoja na mpango wa kitaifa wa usimamizi wa mikoko.
- Kuongezeka kwa misumeno ya kawi na matumizi yake kuvuna mikoko.

